**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MADINI (FUNGU 100) KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

*[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016]*

**DODOMA** **20 APRILI 2020**

**YALIYOMO**

**SEHEMU YA KWANZA** ........ **1**
**1.0 UTANGULIZI** ........ **1**
1.1. Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2019/2020 ........ 2
1.2 Maelezo na Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; ........ 2
1.2.1 Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Chuo cha Madini Dodoma (MRI) ........ 2
1.2.2 Kiwanda cha kutengeneza Mawe ya Nakshi (Dimension Stones) – Ntyuka, Dodoma; ........ 4
1.2.3 Soko la Madini Dodoma na Dar es salaam ........ 7
1.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ........ 11
**SEHEMU YA PILI** ........ **13**
**2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020;** ........ **13**
2.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; ........ 14
2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina 15
2.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka 2019/2020 ........ 17
2.4 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ........ 18
2.4.1 Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ... 18
2.4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato ........ 19
2.4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ........ 20
**SEHEMU YA TATU** ........ 23
**3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** ........ 23
**4.0 HITIMISHO** ........ 28

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Fasili ya 6(9) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati inao wajibu wa kusimamia majukumu yanayotekelezwa na Wizara hii. Aidha, majukumu ya Kamati kuhusiana na Uchambuzi wa bajeti ya kila mwaka ya Wizara inazozisimamia yameelekezwa katika Fasili ya 7(1)(a) ya nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imetekeleza ipasavyo majukumu hayo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kikanuni, Kamati ilifanya kazi zifuatazo:

a) Kutembelea na Kukagua Utekelezaji wa Miradi iliyotengewa Fedha kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 **[*Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016*]**; na

b) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 **[*Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016*].**

## 1.1. Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Madini. Ziara hizo zilifanyika katika Mikoa ya Dodoma na Dar Es Salaam. Lengo la ziara likiwa ni kujionea Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wake. Aidha, Ziara hizi zilifanyika kuanzia tarehe 13 hadi tarehe 17 Machi, 2020.

**Mheshimiwa Spika**, Miradi iliyokaguliwa na Kamati yako kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ni kama ifuatavyo;

i. Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Chuo cha Madini Dodoma (MRI);
ii. Mradi wa Soko la Madini – Dodoma;
iii. Mradi wa Soko la Madini – Dar es Salaam;
iv. Kiwanda cha kutengeneza Mawe ya Nakshi (Dimension Stones) – Ntyuka, Dodoma;

## 1.2 Maelezo na Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

### 1.2.1 Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Chuo cha Madini Dodoma (MRI)

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Usimamizi endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) ulitekeleza kazi mbalimbali ikiwemo Ujenzi wa vituo saba vya umahiri pamoja na ujenzi wa jengo la Taaluma katika Chuo cha Madini (MRI). Awali, Wizara kupitia Mradi ilibainisha Maeneo Saba kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Umahiri kwa ajili ya kutoa mafunzo mbalimbali ya nadharia na baadhi ya mafunzo kwa vitendo kwa ajili ya Wachimbaji Madini Wadogo. Maeneo hayo ni Bariadi, Musoma, Bukoba, Handeni,

Chunya, Mpanda na Songea. Vilevile, Wizara kupitia Mradi imejenga jengo la Taaluma katika Chuo cha Madini (MRI) kwa ajili ya matumizi ya ofisi, madarasa, kumbi za mikutano na ofisi za Chama wa Wachimbaji Madini Wanawake Tanzania (TAWOMA) kwa ajili ya kuendeshea shughuli zao.

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa jengo la Taaluma la Chuo cha Madini (Dodoma) unajengwa na mkandarasi SUMAJKT kwa usimamizi wa mshauri elekezi INTER CONSULT LTD. Mkandarasi SUMAJKT alikabidhiwa eneo la ujenzi lilipo ndani ya Plot 1-10, Block D (Mbwanga Area) lenye ukubwa wa mita za mraba 2,250 mnamo tarehe 14 Julai, 2018 na kazi ya ujenzi ilianza rasmi tarehe 30 Julai, 2018. Ujenzi huu utagharimu kiasi cha **Shilingi 2,863,161,369.00** ikiwa ni pamoja na gharama za ununuzi wa samani mbalimbali pamoja na vifaa vya ofisi.

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa jengo hili unajumuisha kazi za nje na ujenzi wa jengo kuu ambalo litajumuisha ofisi 35 zenye uwezo wa kuchukua watumishi wawili (2) kila moja, vyumba viwili vya mihadhara vyenye uwezo wa kuchukua watu 100 kwa wakati mmoja, chumba kimoja cha kompyuta chenye uwezo wa kuchukua watu 30, chumba kimoja cha mikutano (*Board Room*) chenye uwezo wa kuchukua watu 30 pamoja na ofisi moja ya pamoja (*Pool Office*) yenye uwezo wa kuchukua watu 10 kwa wakati mmoja. Vilevile, jengo hili litakuwa na ofisi ya mitihani 1 na chumba maalum cha kuhifadhia mitihani (Strong room) 1, stoo 1 pamoja na jiko.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea na kukagua jengo la Utawala katika chuo cha Madini na kujionea hali ya utekelezaji wa mradi wa jengo hilo inavyoendelea. Hatahivyo, hadi Kamati ilipotembelea mradi huu ulikuwa umekamilika kwa **asilimia 98**. Aidha, shughuli zilizokuwa zimemilika ni pamoja na ujenzi wa jengo lenyewe, uwekaji mfumo wa

maji safi na maji taka, usimikaji wa mfumo wa umeme, usimikaji wa mfumo wa TEHAMA na usalama (security system), upakaji rangi, uwekaji wa bodi za juu ya dari (ceiling board), uwekaji wa nondo na madirisha ya vioo, uwekaji wa sakafu za kisasa (paving blocks), kusawazisha eneo na kupanda nyasi kuzunguka jengo, upandaji wa miti pamoja na usimikaji wa lifti.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto zilizobainika wakati wa ukaguzi wa mradi huu ni ucheleweshaji wa kumalizika jengo kwa **asilimia 100** kwa kuwa Jengo lilipaswa kumalizika mwaka jana Aprili 2019. Aidha, wakati wa ukaguzi wa mradi Jengo lilionekana kuwa na nyufa katika baadhi ya kuta zinazounda jengo sehemu ya mapokezi. Sambamba na hili, shughuli ambazo zilikuwa hazijakamilika ni pamoja na uwekaji wa vyoo vya walemavu pamoja na mabeseni ya vyooni (sink).

**Mheshimiwa Spika,** Kwa taarifa kutoka Wizara ya Madini wanategemea Jengo hili kukamilika ifikapo mwishoni mwa mwezi Aprili, 2020 na mkandarasi SUMAJKT amelipwa jumla ya **Shilingi 2,721,110,846.74**.

### 1.2.2 Kiwanda cha kutengeneza Mawe ya Nakshi (Dimension Stones) – Ntyuka, Dodoma;

**Mheshimiwa Spika,** Mawe ya Nakshi (*dimension stones*) ni mawe ambayo huchaguliwa na kukatwa katika mwonekano na ukubwa tofauti tofauti kisha hunakshiwa ili kupata vitu mbalimbali kutegemea na mahitaji yaliyopo.

**Mheshimiwa Spika,** uchimbaji hufanyika kwa kutumia mitambo ambayo hutumia waya maalumu wenye ugumu wa hali ya juu kama vile *diamond wire saws* na *diamond belt saws*. Wakati mwingine pia kiasi kidogo cha baruti huweza kutumika ili kutoa mapande ya mawe (*blocks*).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yako ilitembelea Mgodi wa mawe ya nakshi uliopo Ntyuka unaomilikiwa na Ndg. Israel Daud Chunga ambaye ni Mtanzania mwenye elimu ya juu aliyehitimu shahada ya kwanza ya Jiolojia katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na kujionea shughuli mbalimbali za uzalishaji zinazoendelea katika Kiwanda hiki. Mtanzania huyu ameingia ubia wa kuwezeshwa kimtaji na kiteknolojia na kampuni ya Udbhav International Ltd baada ya kupata leseni mwanzoni mwa mwaka 2016. Hadi kufikia mwezi Februari, 2020, Ndg. Israel Daud Chunga alikuwa anamiliki leseni tano zenye jumla ya hekari 23.86 katika Kata ya Ntyuka ikijumuisha na Mtaa wa Ngh'ongh'onha.


**Mheshimiwa Spika,** Katika kusimamia biashara ya mawe ya nakshi, Serikali kupitia Tume ya Madini hufuatilia kwa karibu biashara ya mawe ya nakshi (dimension Stone) na hatimaye hutoa bei elekezi kupitia kitengo cha biashara. *Dimension Stones* zikishapatikana, baadhi husafirishwa hadi jijini Dar es Salaam ambapo hufungwa na kupelekwa nje ya nchi na nyingine husafirishwa hadi Msata Mkoani Pwani ambako kuna mitambo mikubwa ya kukata mawe na hatimaye kutengeneza meza, tarazo, nk ambazo huuzwa hapa nchini. Aidha, masoko ya *dimension stones* yapo ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu kwa kiwango kikubwa hasa yakiwa na ubora unaotakiwa kimataifa. Hata hivyo, soko kubwa la *dimension Stone* lipo nje ya mipaka ya Tanzania.

Lifuatalo ni jedwali linalo onesha mauzo ya *dimension stone* kutoka mgodi wa Ntyuka kwa kipindi cha miaka minne iliyopita;

**uzalishaji na mauzo ya mawe ya *dimension stones* kutoka katika machimbo ya Ntyuka.**

| Year | Weight (Mt) | Value (TZS) | Royalty (TZS) | CIF (TZS) | Total (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| 2016 | 490.00 | 117,357,313.00 | 3,506,050.00 | | 3,506,050.00 |
| 2017 | 1,735.54 | 537,348,533.67 | 17,852,830.00 | 417,440.00 | 18,270,270.00 |
| 2018 | 642.00 | 165,015,136.03 | 4,800,493.25 | 1,202,857.75 | 6,003,351.00 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2019 | 1,313.54 | 340,698,959.00 | 10,220,968.77 | 3,407,244.69 | 13,628,213.46 |
| **Jumla ya Makusanyo** | **4,181.08** | **1,160,419,941.70** | **36,380,342.02** | **5,027,542.44** | **41,407,884.46** |
| **Wastani** | **1,045.27** | **290,104,985.43** | **9,095,085.51** | **1,675,847.48** | **10,351,971.12** |




*mwenendo wa makusanyo ya mawe ya dimension stones kutoka katika machimbo ya Ntyuka.*

**Mheshimiwa Spika,** kutoka mwaka 2016 – 2019 Mgodi umelipa tozo mbalimbali kama vile;

a) Kodi mbalimbali za Halmashauri ya Jiji la Dodoma Shilingi 7,941,994

b) Kodi ya Ongezeko la Mapato (TRA) Shilingi 254,286,016

c) Mfuko wa hifadhi ya Jamii (NSSF) Shilingi 43,968,300

d) Workers Compensation Fund (WCF) Shilingi 2,298,385.20

e) Kununua Ardhi (Eneo) kwa ajili ya machimbo Shilingi 32,410,000.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo katika ziara ya machimbo ya *dimension stone* ya Ntyuka;

a) Uelewa mdogo wa jamii iliyopo inayoenda sambamba na kuwepo kwa matishio kutoka kwa baadhi ya viongozi kutoka

katika Serikali za mitaa kuwa watayafunga machimbo kutokana na hisia kuwa mwekezaji anapata mapato makubwa na mtaa kupata kipato kidogo;

b) Uwepo wa ushuru mwingi kwa madini hayo kwenye Halmashauri ya Jiji na Mtaa, Mfano tozo ya *Building Material Levy* (Shilingi 1,000 kwa tani);

c) Mchango wa "Coorporate Social Responsibility" (CSR) ipo mara mbili:-

   i. Shilingi 500 kwa tani,

   ii. Shilingi 1,000,000 kwa mwaka), na

d) Tozo ya bandarini inayotozwa na Tanzania Shipping Agency Coorporation (TASAC) inakuwa mara mbili kwani, tozo ya kwanza inalipwa kwa TASAC na nyingine unapaswa kutafuta agenti wa kutoa mizigo (clearing and forwarding) na kumlipa pesa nyingine ya kutoa mizigo.

### 1.2.3 Soko la Madini Dodoma na Dar es salaam

**Mheshimiwa Spika,** Masoko ya madini nchini yalianzishwa kufuatia changamoto kubwa iliyokuwa inaikabili Sekta ya Madini kwa kipindi kirefu, hususan ya utoroshaji na biashara haramu ya madini. Changamoto hiyo ilisababisha Serikali kukosa malipo stahiki ya tozo mbalimbali zinazotokana na shughuli za madini. Athari nyingine iliyoambatana na kukosekana kwa masoko ni wachimbaji na wafanyabiashara wadogo wa madini kuuza madini yao kwa kificho na kupelekea kutonufaika na bei halisi ya madini.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilichukua hatua ya kudhibiti hali hiyo ikiwemo kufanya Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 yaliyofanyika mwaka 2017 ambayo yalielekeza kuanzishwa kwa masoko ya madini. Msingi wa uanzishwaji wa Masoko ya Madini, kwa mujibu wa Sheria tajwa

ni kupata takwimu sahihi za mauzo ya madini; kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata soko la uhakika na kupata bei stahiki kwa bidhaa za madini. Masoko hayo pia yameongeza wigo wa ajira za moja kwa moja na zile zisizokuwa za moja kwa moja, kudhibiti uuzaji holela na kupunguza uwezekano wa utoroshaji madini. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Wizara kupitia Tume ya Madini kwa kushirikiana na Wakuu wa Mikoa imeanzisha masoko ya madini 28 na vituo vidogo vya ununuzi 28.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea Masoko ya Madini kwa mkoa wa Dodoma na Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** Soko la madini la Dodoma lilianzishwa tarehe 19 Mei, 2019. Biashara inayofanyika katika soko hili inahusisha madini ya metali hususan dhahabu. Kamati ilibaini kuwa Kabla ya Soko la Dodoma kuanzishwa ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha miezi sita ulikuwa jumla ya **Shilingi 118,401,227.63** (wastani wa **Shilingi 23,680,245.53** kwa mwezi) uliotokana na wastani wa uzito wa **kilogramu 4.22**. Kufuatia kuanzishwa kwa soko hilo, makusanyo yaliongezeka hadi kufikia jumla ya **Shilingi 486,817,451.87** kwa kipindi cha miezi tisa (wastani wa **Shilingi 54,090,827.99** kwa mwezi) uliotokana na uzito wa wastani wa **kilogramu 7.59**. Aidha, Ongezeko hilo limetokana na uwepo wa soko na uwazi katika biashara ya madini hususan dhahabu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa soko la Dodoma changamoto zilizobainika ni pamoja na zifuatazo;

a) Kutokuwepo kwa baadhi ya miundombinu wezeshi kama vile majengo ya kudumu ya kufanyia biashara na majengo kuwa katika hali isiyo ridhisha;
b) Elimu na uelewa mdogo wa kufanya biashara katika masoko rasmi ya madini kwa wachimbaji na wafanyabiashara wadogo wa madini;

c) Upungufu wa wajimolojia na baadhi ya vitendea kazi kwenye masoko ya madini.

**Mheshimiwa Spika,** Soko la madini Dar es Salaam lilianzishwa tarehe 17 Julai, 2019 na lipo kati kati ya Jiji la Dar es Salaam, kwenye Jengo la NHC, Mtaa wa Samora. Biashara inayofanyika katika soko hili inahusisha madini ya aina mbalimbali ikiwemo dhahabu na vito vya thamani.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa kabla ya Soko hili kuanzishwa ukusanyaji wa mapato ulikuwa wastani wa **Shilingi 25,764,040.81** kwa mwezi kwa takwimu za kipindi cha miezi nane kabla ya kuanzishwa kwa soko uliotokana na wastani wa uzito wa **kilogramu 6.36**. Kwa upande wa madini ya vito ukusanyaji wa mapato ulikuwa wa wastani wa **shilingi 44,466,709.23** kwa mwezi kwa takwimu za kipindi cha miezi nane (8) kabla ya kuanzishwa kwa soko**.**

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia kuanzishwa kwa soko hilo, makusanyo yaliongezeka hadi kufikia wastani wa **Shilingi 33,655,304.87** kwa mwezi katika kipindi cha miezi saba tangu soko hilo kuanzishwa ambayo yalitokana na uzito wa wastani wa **kilogramu 4.82**. Aidha, Kamati ilibaini kuwa Ongezeko hilo limetokana na uwepo wa soko na uwazi katika biashara ya madini hususan dhahabu. Kwa upande wa madini ya Vito Ukusanyaji wa mapato ulikuwa wa wastani wa **Shilingi 19,060,448.90** kwa mwezi kwa takwimu za kipindi cha miezi saba (7) baada ya kuanzishwa kwa soko**.**

**Kamati inaipongeza sana Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini kwa kuhakikisha kuwa biashara ya Madini inafanyika kwa uwazi na soko lake kuwa la uhakika, aidha, kwa kiasi kikubwa masoko haya yamepunguza na kudhibiti uuzaji holela wa madini na utoroshwaji wa madini, hivyo Serikali kujipatia mapato na wafanya biashara kupata stahiki zao.**

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa ukaguzi wa soko la madini Dar es Salaam changamoto zifuatazo zilibainika;

a) Kutokuwepo kwa baadhi ya miundombinu wezeshi kama vile majengo ya kudumu ya kufanyia biashara;
b) Elimu na uelewa mdogo wa kufanya biashara katika masoko rasmi ya madini kwa wachimbaji na wafanyabiashara wadogo wa madini;
c) Tozo ya Tanzania Shipping Agency Coorporation – Wakala wa Meli nchini (TASAC)

   Madini yanapozalishwa yanalipiwa mrabaha wa asilimia sita ya thamani ya madini ghafi (raw minerals) yaliothaminishwa na tozo ya ukaguzi ya asilimia moja ya thamani ya madini yaliothaminishwa. Mfanyabiashara wa madini (dealer) anayefanya matayarisho ya kusafirisha madini nje ya nchi (export process) anawajibika tena kulipa asilimia sita ya mrabaha ya thamani ya madini ghafi (raw minerals) yanayosafirishwa nje ya nchi na asilimia moja ya tozo ya ukaguzi ya thamani ya madini yaliothaminishwa na kwa madini yaliyosanifiwa anatozwa asilimia moja ya mrabaha. Hapo hapo, msafirishaji anatakiwa tena alipe asilimia moja 'plus' (1+%) ya TASAC ya kiasi cha madini kilichothaminishwa ili kuweza kupata Kibali kinachotolewa na ofisi ya forodha (Release Order issued by customs office) cha kusafirisha madini hayo nje ya nchi (inspection and clearance fees). Aidha, ndani ya asilimia hiyo moja kuna **asimilia 18** ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ambayo mfanyabiashara anatakiwa kuilipa kwa TASAC kama kodi.

   **Hivyobasi,** malipo haya ya asimilia moja zaidi (1+%) kwa TASAC yanaongeza gharama kubwa kwa mfanyabiashara wa madini ambae angetamani kuongeza thamani madini hayo hapa nchini na hatimaye kusafarisha nje ya nchi. Gharama inazidi kuwa kubwa

katika uendeshaji wa biashara ya madini kwa wafanyabiashara na wauzaji wa madini;

d) Kudaiwa risiti za ki electroniki (EFD) kwa wafanyabishara pindi wanapo nunua mizigo bila kuangalia ununuzi umefanyika kwa wachimbaji wadogo, wa kati ama wakubwa;
e) Kukosekana kwa leseni za masonara kutoka Wizara ya Madini;
f) Usumbufu wa upatikanaji Vibali vya wafanyakazi wanao jihusisha na fani za kutengeneza vito pindi wanapo hitajika kuingia nchini.

## 1.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

i. Wizara ya Madini kushirikiana na mamlaka nyingine kama TASAC (Tanzania Shipping Agency Coorporation) wanapaswa kushirikiana kwa pamoja ili kuangalia namna ya kupunguza Tozo katika kusafirisha madini nje ya nchi, aidha tozo ziwe na kiwango maalumu ambacho mfanyabiashara atatozwa na iwe inalipwa kwa mfumo sawa na kibali cha kusafirisha madini;

ii. Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini wanapaswa kuendelea kutoa elimu kuhusu Sheria na Kanuni kwa wachimbaji wa madini, wafanyabiashara wa madini na wadau wote katika sekta ya madini ili kupunguza adha kwa wafanyabiashara juu ya malipo ya tozo na kodi mbalimbali ambazo kanuni inazitolea ufafanuzi;

iii. Serikali kuangalia namna bora ya upatikanaji wa vibali kwa wadau katika sekta ya madini, kwani upatikanaji wa vibali umeonekana kuwa na urasimu na changamoto za upatikanaji wake kwa wakati;

iv. Kwa kuzingatia Sheria ya madini ya mwaka 2010 na Kanuni za madini za mwaka 2019 kifungu cha 6 kifungu kidogo cha tatu kinampa uhuru mfanyabiashara wa madini anapouza madini yake ndani ya

soko la madini asitozwe kodi ya ongezeko la thamani (VAT) wala kodi ya zuio (withholding Tax) lakini TRA bado wanataka pindi wafanyabiashara wanapo uza madini hawa "*dealers*", sonara na "*brokers*" wengine kutozana VAT. Ni Rai ya Kamati kuwa Wizara kupitia Tume ya Madini wanapaswa kumaliza changamoto hii kwa kushirikiana na mamlaka nyingine ili kuwaelimisha wadau husika juu ya tozo stahiki zinazopaswa kulipwa.

v. Wizara ya Madini inapaswa kushirikiana na Serikali za mikoa katika kuhakikisha kuwa masoko ya madini nchini yapo katika maeneo yenye hadhi stahiki na gharama za upangishaji wa masoko hayo ziwe na bei nafuu kwa kampuni zinazopanga katika masoko hayo. Aidha masoko yanapaswa kuakisi biashara ya madini;

vi. Serikali kuendelea kusimamia na kufatilia wawekezaji binafsi juu ya wafanyakazi wanaofanya kazi katika maeneo ya makampuni mbalimbali ya uzalishaji hapa nchini aidha, wazingatie usalama wa watumishi pamoja upatikanaji wa maslahi ya watumishi kwa ujumla.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI PAMOJA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020;

**Mheshimiwa Spika**, Jukumu la msingi la Wizara ya Madini ni kusimamia maendeleo ya Sekta ya Madini nchini kwa kuweka mifumo thabiti ya utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuhakikisha mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa unaongezeka kazi zilizo tekelezwa na Wizara ya Madini katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Februari, 2020 ni pamoja na: -

i) Kuimarisha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini,
ii) Uanzishwaji na usimamizi wa masoko ya madini,
iii) Kudhibiti utoroshaji wa madini,
iv) Kuwaendeleza wachimbaji wadogo na wa kati wa madini,
v) Kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini,
vi) Kuimarisha ufuatiliaji na ukaguzi wa usalama, mazingira na uzalishaji wa madini katika migodi midogo, ya kati na mikubwa,
vii) Kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini,
viii) Kuendelea kuboresha mazingira ya kuwawezesha wananchi kufaidika na rasilimali madini na kuendeleza rasilimali watu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa kuzingatia mambo makuu matatu ambayo ni:-

a) Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa Fedha 2019/2020;
b) Hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina na;
c) Utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini kwa Bajeti ya mwaka 2019/2020.

## 2.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Madini ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 470,897,011,000.00** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 470,354,398,000.00** zilipangwa kukusanywa kupitia Tume ya Madini, **Shilingi 532,610,000.00** kupitia Chuo cha Madini na **Shilingi 10,003,000.00** kupitia Idara na Vitengo vya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2020 jumla ya **Shilingi 319,025,339,704.73** zimekusanywa ambazo ni sawa na **asilimia 102** ya lengo la makusanyo katika kipindi husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa ya ukusanyaji wa maduhuli ya Wizara na kubaini kuwa ongezeko la makusanyo ya Wizara limetokana na Ongezeko la Ukusanyaji wa Mapato ya Mrabaha kwa Serikali ambapo kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2019 hadi Februari 2020 malengo ya Wizara yalikua ni kukusanya kiasi cha **Shilingi 233,333,333,333.33** Aidha, hadi kufikia mwezi Februari 2020 Wizara ilikua imekusanya kiasi cha **Shilingi 252,419,691,968** sawa na Ongezeko la **asilimia 108.2** la Makusanyo.

**Aidha,** Kamati pia, ilibaini kuwa Ongezeko la Makusanyo ya Wizara pia limetokana na ulipaji faini na malimbikizo ya ada mbalimbali ambapo kwa kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Februari 2020 Lengo la Wizara lilikua ni kukusanya kiasi cha **Shilingi 902,929,333.33** na hadi kufikia Mwezi Februari 2020 Wizara ilikua imekusanya kiasi cha **Shilingi 1,275,358,409.81** sawa na **asilimia 141.2** ya malengo kutokana ulipaji wa adhabu na faini za malimbikizo ya ada kutoka kwa wachimbaji na wafanya biashara ya madini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati vilevile ilibaini kuwa ongezeko la makusanyo pia limetokana na ulipwaji wa ada za kijiolojia na utafiti ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai 2019 hadi Februari 2020 Lengo la Wizara lilikua ni kukusanya **shilingi 10,000,000,000.** Aidha, kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Februari 2020 Wizara imekusanya kiasi cha **Shilingi 10,510,454,265.34** Sawa na Asilimia **105.1** ya Lengo la Makusanyo.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza sana Wizara ya Madini kwa kuvuka lengo la makusanyo kwa mwaka 2019/2020 Aidha, ni rai ya Kamati kuwa Wizara itaendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali madini, usimamizi wa makusanyo na utoroshwaji wa madini ili kuhakikisha malengo yanafikiwa kwa vipindi vyote.**

## 2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliidhinisha Bajeti ya jumla ya **shilingi 49,466,898,200** kwa Wizara ya Madini. Kati ya fedha hizo, **shilingi 7,039,810,200** sawa na **asilimia 14.23** ya Bajeti yote ya Wizara zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, **Shilingi 42,427,088,000** sawa na **asilimia 85.7** ya Bajeti yote ya Wizara zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo inajumuisha mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zake.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Februari 2020, Jumla ya **Shilingi 27,791,986,796** zilipokelewa na Wizara kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizi ni sawa na **asilimia 98.26** ya lengo la Mwaka miezi nane kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 10,587,793,996** sawa na **asilimia 64.27** ni fedha za Matumizi Mengineyo (O.C) na **Shilingi 17,204,192,800** sawa na **asilimia 66.29** zilipokelewa kwa ajili ya kulipa Mishahara.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa Fedha 2019/2020, Fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ilikuwa ni **Shilingi 7,039,810,200.** Aidha, kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2019 hadi Februari 2020, Kamati ilibaini kuwa Wizara iliendelea kutekeleza majukumu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia Fedha za Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali (SMMRP) ambazo ni kiasi cha **shilingi 6,197,175,564.39** zilizotolewa na wadau wakati wa kufunga mradi Disemba 2018. Katika fedha zilizokuwa zimesalia Shilingi 2,839,151,286.14 zimetumika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo zilitumika na mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) kwa ajili ya kukamilisha miradi iliyokuwa inaendelea ikiwa ni pamoja na ukamilishaji wa ujenzi wa Vituo vya Mfano vya Katente na Itumbi, na vya umahiri vya Songea, Mpanda na Chunya. Aidha, Shilingi 3,358,024,278.25 zilitumika kwaajili ya ujenzi wa kituo cha pamoja cha Mirerani, uwekaji wa mfumo wa ulinzi na kamera za usalama pamoja na miundombinu ya umeme kuzunguka ukuta wa Mirerani.

Aidha, kwakuwa Wizara bado haijapata Fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge **Shilingi 7,039,810,200.00** kutoka hazina, kutokana na kuendelea na kukamilisha taratibu za kupata Fedha kwa kutumia mfumo wa sasa ambapo Taasisi husika inawajibika kuwasilisha maombi hazina yakiwa yameambatana na mikataba ya ukandarasi na ankara za madai kuthibistha maombi ya Fedha husika; **Kamati inasisitiza kuwa Serikali ihakikishe kabla ya kwisha kwa mwaka wa Fedha 2019/2020, maombi ya Fedha ambayo yamepokelewa Hazina yawasilishwe kwa Wizara ili Wizara sasa iweze kutekeleza kikamilifu majukumu yake.**

## 2.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Bajeti ya Mwaka 2019/2020 Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Toleo la Januari, 2016 inayoelezea majukumu ya Kamati ya kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa shughuli za Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi bado unahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Maoni ambayo kamati inaamini ni muhimu na yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi ni yafuatayo:-

i. **Uanzishwaji na Uendelezaji wa Masoko ya Madini;** Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali katika kuhakikisha masoko ya madini yanaanzishwa bado kuna changamoto kubwa ya usimamizi masoko hayo, utoaji huduma, miundombinu na ulinzi katika maeneo ya masoko. Kwa muktadha huu, Serikali ihakikishe inaimarisha na kusimamia minada ya mauzo ya madini nchini; na kuhakikisha masoko hayo yanakuwa na wafanyakazi wa kutosha na wenye weledi wa masuala ya madini na masoko ili kuvutia wafanyabiashara wengi wa ndani na nje ya nchi.

ii. **Elimu kwa wachimbaji na wafanyabiashara wa Madini -** Kamati pia iliitaka Serikali iendelee kutoa elimu kwa wafanyabiashara wa madini kuhusu Sheria ya Madini ili kupunguza migogoro mbalimbali kwa wafanyabiashara na wachimbaji wa madini nchini. Changamoto hii bado kwa kiasi kikubwa bado ipo, Elimu kuhusu Sheria na Kanuni za madini bado hazifahamiki kwa wadau husika kwani kumekua na mivutano mingi ya tozo na kodi mbalimbali kwa mamlaka za Serikali pamoja na wachimbaji na wafanya biashara wa Madini nchini.

**Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kamati kuwa Serikali itaendelea kutekeleza maoni na ushauri unao tolewa na Kamati yako.**

## 2.4 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

### 2.4.1 Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wa Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati ilibaini kuwa Mpango na Bajeti wa Mwaka 2020/2021 umezingatia azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujielekeza katika uchumi wa viwanda ambapo **shilingi 6,000,000,000** sawa na **asilimia 85.23** ya Bajeti ya Maendeleo ya **shilingi 7,039,810,177** ya Wizara imeelekezwa katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati *(strategic projects)* ya kuongeza mapato ya Serikali.

Aidha, Maeneo yaliyopewa kipaumbele kwa mwaka 2020/2021 katika Sekta ya Madini na kuzingatiwa katika bajeti ni;

i. Kuimarisha ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali za madini;

ii. Kuimarisha udhibiti na usimamizi wa uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini na kuweka mazingira bora yatakayohamasisha uwekezaji katika sekta ya madini;

iii. Kuendelea kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija,

iv. Kuendelea kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi, kukusanya takwimu za madini na kufuatilia maduhuli yatokanayo na madini,

v. Kuimarisha na kuhimiza uanzishwaji wa masoko ya madini na kuhakikisha upatikanaji wa huduma wezeshi katika masoko hayo,

vi. Kudhibiti utoroshaji na biashara haramu ya madini nchini, Kuendelea kuweka mikakati ya kuimarisha soko la Tanzanite na madini mengine ya vito,

vii. Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini,

viii. Kuimarisha Taasisi zilizo chini ya Wizara;

ix. Kuimarisha shughuli za kitafiti za kijiosayansi na;

x. Kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

**Mheshimiwa Spika, kamati inaridhishwa na malengo na vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka 2020/2021, hata hivyo kamati inatambua kwamba kuwa na malengo ni jambo moja na kufanya juhudi au kutekeleza mikakati kufikia malengo hayo ni jambo lingine. Hivyo kamati inaamini kuwa Serikali itatekeleza mikakati iliyonayo kwa ufanisi ili kufikia malengo iliyojiwekea kwa manufaa ya Taifa.**

### 2.4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Madini inakadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 547,745,866,597** kwa mwaka wa Fedha 2020/2021. Kamati ilifanya ulinganisho wa bajeti hii ya makadirio ya mapato na kubaini kuwa mwaka 2019/2020 makadirio ya mapato yalikua kiasi cha **Shilingi 476,380,613,492** hivyo sawasawa na ongezeko la **asilimia 14.98 kwa** Mwaka 2020/2021. Kati ya Fedha zitakazokusanywa, **Shilingi 526,732,550,000** sawa na **asilimia 96.16** zitakusanywa na kuwasilishwa Hazina na **Shilingi 21,013,316,597** sawa na **asilimia 3.84** zitakusanywa na kutumika na Taasisi na Wakala zilizo chini ya Wizara. Jedwali Lifuatalo linaonesha mchanganuo wa maduhili hayo.

**Maduhuli yatakayokusanywa na Kuwasilishwa Hazina**

| Na. | Taasisi | Makadirio ya Maduhuli |
|---|---|---|
| 1 | Idara na Vitengo vya Wizara | 10,003,000.00 |
| 3 | Tume ya Madini | 526,722,547,000.00 |
| **JUMLA** | | **526,732,550,000.00** |
| **Maduhuli yatakayokusanywa na Kutumika na Taasisi** | | |
| 1 | Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania | 508,386,000.00 |
| 2 | Shirika la Madini la Taifa | 19,431,609,797.00 |
| 3 | Chuo cha Madini | 913,320,800.00 |
| 4 | Kituo cha Jemolojia Tanzania | 160,000,000.00 |
| **JUMLA** | | **21,013,316,597.00** |

***Chanzo; Taarifa ya Makadirio ya Mapato ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021***

### 2.4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara ya Madini inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 62,781,586,000** ikilinganishwa na **Shilingi 49,466,898,200** zilizoidhinishwa na Bunge katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 hivyo makadirio haya ni sawa na ongezeko la **asilimia 26.92.** Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kuwa, Nyongeza ya Fedha hizo imetokana na kuongezeka kwa fedha za Miradi ya Maendeleo pamoja na Fedha za Matumizi ya Kawaida. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa Serikali imeongeza fedha hizo kwa Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa ajili ya ujenzi wa miundominu ya ofisi, hifadhi za sampuli ya miamba ya madini, ununuzi wa vifaa na mitambo ya utafiti pamoja na uimarishaji wa mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na rasilimali madini.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara imetengewa kiasi cha **Shilingi 8,500,000,000** ikiwa ni Bajeti ya Miradi ya Maendeleo. Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kuwa, Kwa mwaka wa

Fedha 2019/2020 fedha zilizotengwa kwaajili ya miradi ya maendeleo ilikuwa ni **Shilingi 7,039,810,200** hivyo ukilinganisha na bajeti ya mwaka **2020/2021** Fedha za miradi ya maendeleo zimeongezeka kwa **asilimia 20.74**.

**Mchanganuo wa Fedha za Miradi ya Maendeleo**


| Kifungu | Maelezo ya Kifungu | Mchanganuo kwa kila Taasisi | Kiasi | Jumla ya Mradi |
|---|---|---|---|---|
| **2001 - 1119** | Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini | Wizara | 2,400,000,000 | **8,500,000,000** |
| | | Tume ya Madini | 2,180,000,000 | |
| | | GST | 2,400,000,000 | |
| | | STAMICO | 1,520,000,000 | |

***Chanzo; Taarifa ya Makadirio ya Mapato ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021***

**Mheshimiwa Spika,** Wizara inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 54,281,587,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Bajeti hii inajumuisha **Shilingi 33,235,659,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) kwa Wizara na Taasisi zake ambayo ni sawa na **asilimia 61.23** ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Aidha, Wizara imetenga **Shilingi 21,045,927,000** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake ambayo ni **asilimia 38.77** ya bajeti ya Wizara ya Matumizi ya Kawaida.

**MWENENDO WA BAJETI YA WIZARA YA MADINI KUANZIA MWAKA 2017/2018 HADI 2019/2020**

| **Mwaka** | **2017/2018** | **2018/2019** | **2019/2020** |
|---|---|---|---|
| O.C | 13,912,800,000 | 20,953,262,992 | 25,953,263,000 |
| P.E | 16,749,567,000 | 18,334,255,000 | 16,473,825,000 |
| Matumizi ya Kawaida | **30,662,367,000** | **39,287,517,992** | **42,427,088,000** |
| Maendeleo | 21,783,000,000 | 19,620,964,000 | 7,039,810,200 |
| JUMLA YA BAJETI | **52,445,367,000** | **58,908,481,992** | **49,466,898,200** |




Chanzo; Taarifa ya Bajeti ya Wizara ya Madini 2019/2020

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yako imetekeleza majukumu yake ya msingi yaliyoainishwa katika Kanuni ya 98 (1) na (2) pamoja na kanuni ya 117(11a) ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. Hivyo basi, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao kwa Wizara ya Madini;

### 3.1 Tozo ya 1% inayotozwa na Wakala wa Meli Nchini Tanzania (TASAC)

Kwa kuwa Wafanyabiashara wa madini wanapo safirisha madini nje ya nchi wamekuwa wakitozwa kodi ya 1% na Wakala wa Meli nchini Tanzania (TASAC), jambo ambalo sio tu limekuwa likiongeza gharama kwa wafanyabiashara bali pia limekuwa likiwakatisha tamaa na hivyo kuikosesha Serikali mapato; Kamati inaamini kwamba kupunguzwa ama kuondolewa kabisa kwa kodi hii kutachochea ukuaji wa biashara ya madini yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi. Hivyo basi, Kamati inaishauri Wizara ya Madini kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali ikiwemo TASAC (Tanzania Shipping Agency Coorporation) kuangalia namna ya kupunguza Tozo hiyo ya kusafirisha madini nje ya nchi. Aidha, kiwango cha tozo ambacho mfanyabiashara atatozwa kiwe rafiki na kilipwe kwa mfumo sawa na kibali cha kusafirisha madini;

### 3.2 Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Wafanyabiashara wa Madini Katika Masoko ya Madini;

Kwa kuzingatia Sheria ya madini ya mwaka 2010 na Kanuni za madini za mwaka 2019 kifungu cha 6 kifungu kidogo cha tatu kinampa haki mchimbaji mdogo wa madini anapouza madini yake ndani ya soko la madini asitozwe kodi ya ongezeko la thamani (VAT) wala kodi ya zuio (withholding Tax). Hatahivyo katika soko hilo hilo kanuni ipo kimya kwa "*dealers*" na "*brokers*" ambao nao wanauza na kununua madini katika

soko hilohilo; na hivyo wafanyabiashara hawa pindi wanapo uziana madini Mamlaka ya Mapato (TRA) inawataka kutozana kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Ni Rai ya Kamati kuwa Wizara na Tume ya Madini kwa kushirikiana na mamlaka nyingine wanapaswa kumaliza changamoto hii kwa kushirikiana kuweka uwanja sawa wa ulipaji kodi na hatimaye kuwaelimisha wadau husika juu ya tozo stahiki zinazopaswa kulipwa.

### 3.3 Uendeshaji na Uratibu wa Masoko ya madini

Kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazo kabili masoko ya madini kwa wafanyabiashara wa Madini katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Changamoto hizi zimejumuisha, masoko kutokuwa kwenye maeneo stahiki ya kibiashara, baadhi ya majengo ikiwemo ya Serikali kuwatoza kodi kubwa wafanyabiashara, gharama kubwa za uendeshaji masoko hayo, mlolongo wa kodi n.k. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara na Tume ya Madini kushirikiana kwa karibu na Mamlaka za mikoa ili kuainisha maeneo stahiki yenye mwamko na hadhi za kibiashara ili kutumika kama masoko. Aidha, kushirikiana na mamlaka nyingine zinazo miliki majengo yanayo tumika kama masoko ya madini kupunguza kodi ili kuwaondolea wafanyabiashara wa madini mzigo mkubwa wa gharama za uendeshaji. Sambamba na hili kupunguza changamoto za mlolongo wa kodi kwa wafanyabiashara kutachochea ufanisi wa dhana hii njema ya masoko ya madini na kuondoa kabisa changamoto ya utoroshwaji wa madini.

### 3.4 Miundombinu ya barabara Kiwira- Kabulo

Wizara ya Madini kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI zinapaswa kuchukua hatua za haraka katika kuhakikisha zinamaliza changamoto za utengenezaji wa barabara katika mradi wa Kiwira-Kabulo kwakuwa kutotengenezwa kwa barabara hii kunaliingizia hasara Taifa kutokana na uzalishaji wa makaa ya mawe katika mgodi huo kufanyika kwa gharama kubwa;

### 3.5 Masharti ya Vyeti Vya Kitaaluma kwa Waongeza Thamani Madini (Craftmen)

Kamati inaishauri Serikali kuona uwezekano wa kuondoa sharti la vyeti vya taaluma kwa wachakata madini (craftmen) wanaoingizwa nchini kutoka kwenye nchi zilizobobea kwenye sekta ya usonara kwani kwenye eneo hili mfumo unaotumika kuwapata wataalamu wengi kwenye nchi hizo ni ule wa kurithishana ujuzi kutoka kizazi kimoja hadi kingine badala ya taaluma ya darasani. Hivyo kutarajia wataalamu hawa kuwa na vyeti ni kuendelea kuwanyima fursa watanzania kupata utaalamu huu na hivyo kukosa wataalamu wazalendo. Aidha, sambamba na hili, Serikali inapoteza makusanyo ya mapato kupitia shughuli hizi za uongezaji wa thamani madini;

### 3.6 Usimamizi wa Usalama wa Wafanyakazi kwa Makampuni ya Madini na Tume ya Madini

Kwa kuwa Kamati ilibaini kuwepo kwa malalamiko ya wafanyakazi katika makampuni ya uchimbaji madini ikiwemo suala la usalama katika maeneo ya kazi na kufanyishwa kazi kwa muda mrefu; na vilevile baadhi ya watumishi wa Tume ya Madini wanaosimamia maslahi ya Serikali katika madini wamekuwa wakihujumiwa, kutishiwa maisha na wakati mwingine kuhatarisha ajira zao. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kusimamia na kufatilia kwa karibu mienendo ya wawekezaji binafisi hususan kwenye eneo la usalama wa wafanyakazi ili kuhakikisha kuwa kanuni za usalama kwa watumishi pamoja upatikanaji wa maslahi ya watumishi kwa ujumla zinazingatiwa.

### 3.7 Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

Pamoja na ongezeko la mapato kwa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) bado Shirika limekuwa likikabiliwa na changamoto mbalimbali kupitia uwekezaji wake katika miradi mingi. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na ufinyu wa mtaji, miundombinu isiyofaa ya barabara kuelekea

kwenye mgodi wa makaa ya mawe Kiwira- Kabulo, kutokamilika kwa umiliki wa hisa katika kampuni ya makaa ya mawe ya Kiwira pamoja na madeni makubwa sana ya wafanyakazi. Aidha, kwa upande wa kampuni ya STAMIGOLD ambayo ni kampuni tanzu ya shirika la STAMICO, kumekuwa na changamoto za gharama kubwa sana za uendeshaji na uzalishaji kutokana na matumizi ya mafuta mazito ya diesel, ufinyu wa mtaji katika shughuli za uchorongaji, upanuzi wa mgodi na uchenjuaji wa madini, uchakavu wa mitambo na miundombinu, mzigo mkubwa wa madeni kwa shirika unaofikia 39.37 bilioni; na ucheleweshwaji wa marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani. Kutokana na changamoto hizi, **Kamati inaishauri Serikali kwa mara nyingine tena, Kuiangalia STAMICO kwa jicho la kipekee ili iweze kuwa chachu ya kuendeleza sekta ya Madini hapa nchini kwa kuipatia mtaji utakaowezesha Shirika kujikwamua katika uendelezaji wa migodi inayoisimamia.**

### 3.8 Wajibu wa Makampuni ya Uchimbaji kwa Jamii zinazowazunguka

Kwakuwa Serikali imeendelea kusimamia kwa umakini mkubwa kuhakikisha makampuni mbalimbali ya madini nchini yanatoa sehemu ya mapato yake kisheria kuhudumia maeneo ya jamii zinazo yazunguka. Na kwakuwa, Kamati imebaini kuwa kwa sehemu kubwa kampuni za wazawa zimekuwa nyuma sana katika utekelezaji wa suala hili. Hivyobasi, kamati inaishauri Serikali kupanua wigo wa utekelezaji wa jukumu hili. Wigo huu sasa ushirikishe na kampuni nyingine zenye mikataba na kampuni za uchimbaji za kutoa huduma mbali mbali ili kuongeza ufanisi wa kimatokeo kwa jamii husika.

### 3.9 Uendelezaji wa wataalamu katika masuala ya Jiolojia

Kwa kuwa Wakala wa Jiolojia nchini (GST) imeendelea kukabiliwa na changamoto ya upungufu wa wataalamu wenye taaluma stahiki kama vile wakemia, wajiolojia, na wahandisi wa jiolojia; Kamati inaendelea

kuishauri na kuisisitiza Serikali kuwekeza kwa kutoa fursa za masomo kwa wananchi na watumishi mbalimbali katika taaluma hizo ili kuweza kupata wataalamu. Aidha, Serikali iboreshe maslahi ya watumishi wenye taaluma hizo kwani kazi wanazofanya ni kubwa na zina manufaa makubwa kwa Taifa.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe Mhe. Job Yustino Ndugai (Mb) Spika, Dr. Tulia Akson (Mb) Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliongoza Bunge hili kwa weledi mkubwa. Tunawaombea afya njema na uzima katika kuendelea kutekeleza majukumu mliyopewa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati yako. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Mohamed Juma Khatib, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Ally Mohamed Keissy, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb - Mjumbe
11. Mhe. John Wegesa Heche, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Hamoud Abuu Jumaa, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Msukuma Joseph Kasheku, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Yosepher Ferdinand Komba, Mb - Mjumbe
18. Mhe. James Kinyasi Millya, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb - Mjumbe

20. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Hamida Mohamed Abdallah, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Kiza Hussein Mayeye, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Frank George Mwakajoka, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Abdallah Ally Mtolea, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** nitoe pia shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati kwa Mhe. Doto Mashaka Biteko(Mb) – Waziri wa Madini, Mhe. Stanslaus Haroun Nyongo(Mb) - Naibu Waziri wa Madini pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Profesa Simon Msanjila kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Steven Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto pamoja na Makatibu wa Kamati Ndg. Felister Mgonja na Ndg. Herman Edgar Berege kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 100 Wizara ya Madini kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja ambayo ni **Shilingi 62,781,586,000.**

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuwasilisha na Naunga mkono hoja.

Dunstan Luka Kitandula
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**

20 Aprili, 2020